*Kioo cha Lugha, Juz. 22(1), 112-122*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v22i1.7

# Matumizi ya Fantasia katika Fasihi ya Kiswahili Yanavyoibua, Kujenga na Kuwasilisha Dhamira

*Gerephace Mwangosi*[1]


## Ikisiri

Makala hii imechunguza namna kipengele cha fantasia katika fasihi ya Kiswahili kinavyoibua, kujenga na kuwasilisha dhamira. Lengo la makala hii ni kuchunguza namna kipengele cha fantasia kinavyotumika kuibua, kujenga na kuwasilisha dhamira katika riwaya ya Kiswahili. Data za msingi zilipatikana katika riwaya teule ya *Kusadikika* kwa mbinu ya usomaji makini. Nyaraka zilizotumika kufafanua na kuthibitisha data za msingi zilipatikana kwa mbinu ya kielektroniki na kimaktaba. Uchambuzi na mjadala wa data uliongozwa na Nadharia ya Semiotiki. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kushughulika na ishara pamoja na uashiriaji katika kazi za fasihi. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa mbinu ya kimaelezo. Matokeo yameonesha namna msuko wa fantasia katika kitabu teule unaivyoibua dhamira zinazolenga kuifunza, kuiimarisha na kuiweka jamii pamoja katika misingi imara ya utamaduni, siasa na uchumi. Dhamira zilizoibuliwa zinawasilisha matendo ya msingi ya binadamu yanayojidhihirisha katika nyanja zote za maisha na maendeleo yake. Kwa hiyo, makala hii inapendekeza kuwa utafiti ufanyike zaidi katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili kuhusu matumizi ya fantasia yanavyofumbata masuala ya uchumi, siasa, utamaduni, falsafa na itikadi za jamii.


## 1.0 Utangulizi

Makala hii imechunguza namna matumizi ya fantasia yanavyoibua dhamira katika fasihi ya Kiswahili kwa kurejelea riwaya teule ya *Kusadikika*. Fantasia ni hali ya kuwapo kwa mambo ya undotondoto katika kazi ya fasihi yasiyotarajiwa kutokea katika maisha ya kawaida (Herman, 2012). Mambo hayo huwa yamesheheni masuala ya kinjozi, uajabuajabu ama majitu yanayotisha yenye nguvu zisizo za kawaida. Pia, ni dhana inayotumiwa kueleza kazi ya fasihi ambayo ina sifa zinazokiuka hali halisi ya mambo na maisha ya binadamu, utamaduni na mazingira yake (Wamitila, 2002). Kazi hizo huchota malighafi yake kutoka katika tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili.

Fantasia ni ishara mojawapo inayodhihirisha ukuaji wa kiutambuzi katika kazi za fasihi. Pia, husaidia kumjenga na kumwingia mhusika katika ulimwengu

[1] Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu Katoliki cha Mbeya.
Baruapepe:gerephace.mwangosi@cucom.ac.tz

wa fikra za kisanaa zilizowasilishwa kinjozi kuhusu mahali ambapo mtu hajawahi kufika maishani mwake (Mutua na Furaha, 2014). Matumizi ya fikra za kinjozi ndiyo ulimwengu wa kifantasia ambao ni muhimu katika kazi za fasihi. Pia, fantasia hutumika katika kazi za kinathari ambazo huwa na mandhari ya ajabu, matukio magumu kukubalika katika hali ya kawaida na hata wahusika wasioweza kupatikana katika hali halisi (Herman, 2012). Aidha, fantasia inaweza kuhusisha baadhi ya wahusika wasio wa kawaida kama vile mazimwi, majini, mashetani, vitu na viumbe wengine ambao hawawezi kupatikana katika hali ya ukweli unaoweza kuthibitishwa. Kwa upande mwingine, fantasia hujidhihirisha katika vipengele vya fasihi simulizi kama vile visapanda, visaviini, visasili, majigambo na mwingiliano-tanzu (Senkoro, 2011). Mojawapo ya matumizi ya fantasia ni kuijengea hadhira taharuki, kufanikisha ujenzi wa mandhari na kuvuta usikivu kwa hadhira.

Katika fasihi, fantasia inatumika kuelezea kitu kinachowakilisha kingine. Kuwakilisha huku kunaweza kutokana na uhusiano uliopo baina ya vitu hivyo au uwezo wake wa kuibua fikra katika akili ya msikilizaji au msomaji. Pia, inaweza kuhusishwa na muktadha mpana wa kimwingilianomatini unaovuka mipaka ya jamii moja kulingana na jinsi kazi hizo zinavyohusiana na kuingiliana (Wamitila, 2008). Muktadha huo unachukulia kuwa matumizi ya fantasia katika fasihi ni chombo cha kiulimwengu katika utekelezaji wa majukumu yake. Kazi fulani inaweza kuashiria jambo lililopo ndani na nje ya jamii ya msanii. Uchambuzi wa kazi kama hiyo hutegemea sana uelewa wa kutosha kuhusu mifumo ya jamii na mabadiliko ya mazingira yake (Wanjala, 2013). Jukumu la mchambuzi ni kujenga uwezo wa kuona tabia, silka, itikadi, utamaduni na uhusiano wa matabaka katika jamii. Hali hiyo humpa urahisi wa kupata uzito wa dhana na picha za maneno yaliyotumika katika utanzu unaohusika.

Riwaya teule ya *Kusadikika* iliandikwa na Shaaban Robert (1951) nyakati za utawala wa kikoloni barani Afrika. Kwa vyovyote vile, inawezekana kuwa uandishi wake ni matokeo ya masuala ya siasa, uchumi, utamaduni na mazingira ya kipindi hicho cha kabla ya uhuru wa Tanzania (Tanganyika) kupatikatika. Matumizi ya fantasia katika uandishi wake yameibua dhamira zilizojengwa kwa kutumia uzoefu na vielelezo vinavyosawiri hali na maisha ya jamii husika. Pia, ni mojawapo ya vielelezo vinavyoonesha namna mwandishi alivyoyaakisi na kudokeza masuala yaliyowakabili wananchi katika kipindi cha uandishi wa riwaya yake. Kwa hiyo, makala hii imechunguza namna kipengele cha fantasia kinavyotumika kuibua na kuwasilisha dhamira katika riwaya teule ya *Kusadikika*.

## 2.0 Nadharia na Methodolojia ya Utafiti

Makala hii imechunguza namna kipengele cha fantasia kinavyoibua dhamira katika fasihi ya Kiswahili. Data za msingi zimepatikana katika riwaya ya *Kusadikika* kwa mbinu ya usomaji makini. Nyaraka zilizotumika kufafanua na kuthibitisha data za msingi zilipatikana kwa mbinu ya kieletroniki na kimaktaba. Matokeo ya uchunguzi yamewasilishwa kwa mbinu ya kimaelezo. Uchambuzi na

mjadala wa data uliongozwa na Nadharia ya Simiotiki iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure na Charles Pierce (Mark, 1995). Nadharia hii inahusu taaluma ya mfumo wa alama katika mawasiliano ya kutumia lugha. Dhima yake ni kushughulika na ishara pamoja na uashiriaji katika kazi za fasihi. Ishara zinazojitokeza katika fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii (Nazarova, 1996). Aidha, binadamu ndiye mtengenezaji wa ishara zinazotumika katika mawasiliano yake. Kwa hiyo, hadhira hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri yake juu ya alama na ishara zinazotumika.

Barthes (1994) aliainisha Nadharia ya Simiotiki katika misimbo mbalimbali. Misimbo hiyo ni ule wa kiseme, kihemenitiki, kimatukio, kirejelezi na ishara. Msimbo wa kiseme hutumika kuelezea elementi nasibishi za kisemantiki. Pia, huonesha elementi zinazomwezesha msomaji kupata picha ama yaliyomo katika kazi ya fasihi inayohusika. Msimbo huu ulimsaidia mtafiti kujenga picha kutokana na matumizi ya fantasia yalivyojitokeza katika riwaya teule. Kwa upande mwingine, msimbo wa kihemenitiki unahusu neno au maneno katika mfumo wa lugha kutoa fununu ya maana ya neno au maneno (Wamitila, 2002). Kwa kurejelea misingi ya msimbo huo, mtafiti alipata uelewa mpana wa kubaini namna matumizi ya kipengele cha fantasia yanavyoibua dhamira katika riwaya teule ya *Kusadikika*.

Msimbo wa matukio unahusisha matukio yanayofuatana kiathari na kiusababishi katika kazi za fasihi. Msimbo huo ulimruhusu mtafiti kuchunguza mfuatano wa matukio ili kubaini namna matumizi ya fantasia yanavyoibua dhamira katika kitabu teule. Aidha, msimbo wa kiishara unahusu jinsi msikilizaji au msomaji anavyovumbua maana kiishara katika kazi za fasihi (Ntarangwi, 2004). Kwa kurejelea kitabu teule, msimbo huu ulimsaidia mtafiti kuelewa ishara na namna kipengele cha fantasia kilivyotumika kuelezea kitu kilivyokusudiwa. Kwa upande mwingine, msimbo wa kirejelezi hujengwa na viashiria vya utamaduni. Msimbo huu ulimsaidia mtafiti kujua mambo ya kiutamaduni yalivyobainishwa katika fantasia zilizoibua dhamira mbalimbali katika riwaya teule.

Wamitila (2002) alionesha kwa mifano namna nadharia teule inavyosaidia kupatikana kwa maana zaidi ya moja baada ya kuvunjavunja matini katika sehemu ndogondogo alizoziita leksia. Pia, alieleza kuwa kila leksia ina maana zaidi ya moja anazozipata msikilizaji au msomaji wa matini inayohusika. Nadharia hii inaungwa mkono na wataalamu wengi wa lugha kutokana na msingi wake mkuu wa kuhusisha vitu. Pia, inatumika katika tahakiki nyingi na huonesha namna inavyokubalika baada ya kufikia malengo ya kazi husika. Kwa mfano, Khamis (2013), Kimambo (2015) na Wahida (2016) waliitumia nadharia hii katika uhakiki wa vipengele vya lugha katika kazi za fasihi na kufikia malengo ya kazi yao.

Omary (2011) aliitumia nadharia hii katika uchunguzi wa kipengele cha lugha kwa kurejelea vitabu vya *Kichomi* na *Karibu Ndani*. Omary alizichunguza ishara zilizojitokeza katika vitabu teule kama matokeo ya mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii yake. Pia, alimchunguza mwandishi kama mtengenezaji wa

alama mbalimbali ambazo zilitumika kuwasilisha dhamira zake. Utafiti huu kama wa Omary ulimfanya mtafiti kumchunguza mwandishi teule kama mtengenezaji wa fantasia zinazoibua dhamira mbalimbali katika kitabu chake. Uchunguzi wa fantasia ulizingatia kuwa msanii hufikiri kwa kutumia alama zinazowasilishwa kupitia mfumo wa maneno, picha na matendo ya wahusika. Mtafiti aliweza kubaini dhamira mbalimbali kwa kurejelea matumizi ya fantasia yaliyopatikana katika riwaya teule.

Pia, Rajabu (2012) aliitumia Nadharia ya Semiotiki katika uchunguzi wa misemo ya Kiswahili katika vazi la fulana. Katika utafiti wake, alieleza kuwa hadhira hubaini maana ya kazi fulani ya fasihi kupitia ubunifu na tafsiri zake juu ya ishara zilizotengenezwa na msanii. Utengenezaji wa maana hutegemea muktadha wa mnyambulishaji wa ishara zinazotumika katika kazi inayowasilishwa. Katika makala hii, mtafiti aliitumia nadharia hii kuchunguza matumizi ya fantasia yanavyoibua dhamira katika riwaya teule. Uchunguzi ulizingatia kuwa kitu chochote kitakuwa fantasia kama watu watakifasiri kwa niaba ya kitu kingine. Huu ndio msingi wa uteuzi wa nadharia hii katika uchunguzi wa matumizi ya fantasia yanavyoweza kuibua dhamira katika kazi za fasihi.

Kwa ujumla, uchambuzi wa kipengele cha fantasia namna kinavyoibua dhamira katika riwaya teule ulizingatia kuwa binadamu anafikiri kwa kutumia alama zinazojidhihirisha katika mfumo wa maneno, picha, sauti na matendo. Mtafiti alichunguza namna kazi za fasihi zinavyotumia kipengele cha fantasia kuibua dhamira kupitia maneno, taswira, picha na matendo kurejelea tabia za binadamu katika riwaya teule. Kwa kufanya hivyo, mwandishi wa riwaya teule aliwekwa katika muktadha wake wa kawaida kwa lengo la kujua namna maneno, picha, sauti na matendo yalivyojengwa kifantasia ili kuibua dhamira katika riwaya teule.

## 3.0 Matumizi ya Fantasia Yanavyoibua Dhamira katika Riwaya Teule

Matokeo ya utafiti yaliyowasilishwa katika kipengele hiki yameonesha namna matumizi ya fantasia yanavyoibua dhamira katika riwaya teule ya *Kusadikika*. Pia, yanaonesha jinsi kipengele cha fantasia kinavyotumika kama wakala wa kuibua dhamira zinazoakisi muktadha wa jamii ya mwandishi. Sehemu inayofuata imewasilisha namna matumizi ya fantasia yanavyoibua dhamira katika riwaya teule.

### 3.1 Fantasia Inayoakisi Ulafi wa Taifa la Majuju

Katika riwaya teule ya *Kusadikika* matumizi ya fantasia yameibua dhamira mbalimbali zinazoakisiwa katika jamii. Mojawapo ya fantasia iliyotumika kuibua dhamira ya ulafi na ubadhirifu wa mali za umma katika kitabu teule ni ile inayoonesha ulafi wa mfalme Jeta katika taifa la Majuju. Dhamira ya ulafi, uchu na ubadhirifu wa mali ya umma katika jamii imeibuliwa kifantasia kupitia mienendo, tabia na matendo ya mfalme Jeta. Matumizi ya fantasia yanajidhirisha

vyema namna yanavyoibua dhamira zilizobainishwa pale mwandishi anapoeleza kuwa Majuju ni taifa lafi. Pia, anaeleza kuwa kila kitu kigumu kinachojulikana duniani kilikuwa laini kama mkate kati ya meno ya Majuju, na kilicho kichungu kilikuwa kitamu kama asali katika maonjo yao. Maelezo haya yanaonesha namna yalivyowasilishwa kifantasia kuibua dhamira ya ulafi, uchu na ubadhirifu wa mali za umma katika jamii. Mwandishi anaeleza:

> Majuju ni taifa lafi na litishalo kabisa. Kila kitu kigumu kijulikanacho duniani kilikuwa laini kama mkate kati ya meno ya Majuju; na kilicho kichungu kilikuwa kitamu kama asali katika maonjo yao. Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta alimkuta amekaa kitako midomo wazi. Mto mrefu na mpana ulikuwa ukimiminika katika kinywa chake kikubwa sana. Tone la maji hata moja halikupata nafasi ya kukiepa kinywa hicho. Tani milioni moja za miamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo na milioni nyingi za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji humo kinywani kila baada ya dakika tano. Lakini, kila dakika moja, Jeta alilia; kiu, njaa, kiu, njaa (kur. 23 – 24).

Kifungu hiki kinaonesha matumizi ya fantasia yanavyoibua dhamira mbalimbali, ikiwamo ya ubadhirifu wa mali za umma kupitia kwa mfalme Jeta. Matumizi ya fantasia katika makala hii yalizingatia misingi ya Nadharia ya Simiotiki kuwa lugha anayoipata mtu huwa ni matokeo ya mwingiliano wa jamii. Kwa mfano, inaelezwa namna mto mrefu na mpana ulivyokuwa ukimiminika katika kinywa chake kikubwa sana, na tani milioni moja za miamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo na milioni nyingi za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji humo kinywani. Jeta alikuwa akimeza mamilioni ya chuma, magogo, samaki na mto kila baada ya dakika tano. Maelezo haya yanaonesha kuwapo kwa kasi kubwa ya ubadhirifu inayofanywa na baadhi ya viongozi wasio waadilifu katika jamii. Ubadhirifu wa mali za umma ni hatari kwa ustawi wa taifa na ni ishara ya kuangamia kwa maendeleo ya uchumi na watu (Mukandala na Gasavasi, 2000). Ubadhirifu ni hatari kwa ustawi na uendelevu wa uchumi wa jamii na taifa.

Aidha, licha ya kuwa tani milioni moja za miamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo na milioni nyingi za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji humo kinywani kila baada ya dakika tano; lakini, kila dakika moja, Jeta alilia: kiu, njaa, kiu, njaa (uk. 24). Kwa hali ya kawaida, si rahisi vitu vinavyoelezwa kuingia katika kinywa cha mtu. Kinachoelezwa hapa ni kuwapo kwa kasi iliyopindukia ya ubadhirifu wa mali za umma inayofanywa na baadhi ya viongozi katika jamii. Hatua kali za kisheria na kikatiba zinapaswa kuchukuliwa ili kupambana na viongozi wanaotumia madaraka vibaya (Tehenan, 2003). Ubadhirifu wa mali ya umma unaathiri misingi na mwendo wa maendeleo ya taifa na watu wake. Tabia ya viongozi kubadhiri mali ya umma imeendelea kuimarika katika nchi nyingi za Afrika hata kabla mataifa hayo hayajaanza kupata uhuru

(Nyerere, 1974). Hali hii imechangia kufifia na kuanguka kwa miundombinu na huduma muhimu nchini.

Pia, matumizi ya fantasia yameibua dhamira ya uchoyo na ulafi kupitia kwa mfalme Jeta aliyetaka kunufaika peke yake kutokana na adhabu aliyokuwa amepewa Kabuli. Jeta hakutaka kushirikiana na wawindaji ambao walimkata Kabuli. Matokeo ya kutaka kufanya hivyo, yalisababisha vita baina ya majeshi ya mfalme na wawindaji. Mwandishi anaeleza kuwa vita baina yao vilisababisha kuangamizwa kwa kila kilichokuwa na uhai na kuwapo kwa uharibifu mkubwa wa miundombinu na mali (uk. 24). Ulafi wao ulisababisha vita vilivyochochea uharibifu wa miundombinu na vifo vya raia. Viongozi wanapaswa kutumia madaraka na dhamana waliyopewa kwa manufaa ya umma badala ya kuendekeza ulafi na uchoyo (Ramadhan, 2018). Aidha, ni wajibu wa viongozi kuandaa namna bora ya kuwajenga wananchi katika misingi imara ya kumudu changamoto za kimaisha na kimazingira kwa mbinu za wazi na uhakika. Pia, wanapaswa kuyaepusha mataifa yao katika migogoro isiyokuwa ya lazima.

### 3.2 Fantasia Inayoonesha Ukosefu wa Miundombinu ya Usafirishaji na Uchukuzi

Mwandishi ametumia fantasia kuibua dhamira ya ukosefu wa miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi katika jamii. Fantasia iliyotumika kuibua dhamira hiyo ni ile inayoonesha namna Kabuli alivyosafirishwa kwa kasi ya mkondo wa mto kwa muda wa saa 10 tu badala ya miaka kumi kwa miguu. Katika kuwasilisha dhamira hiyo, Kabuli alielezwa kuwa mahali alipoteleza na kutumbukia majini mpaka alipofika ilikuwa ni mwendo wa miaka kumi kwa miguu, lakini kwa nguvu ya mkondo wa mto alifika kwa mwendo wa saa kumi, kila mwaka mmoja kwa saa moja tu (uk. 32). Kwa kawaida, hakuna uwiano kati ya saa alizosafirishwa kwa kasi ya mkondo wa mto dhidi ya ule ambao angetumia kwa miguu. Matumizi ya fantasia hiyo yanaonesha kuwa uhai na maendeleo ya taifa hutegemea sana kuwapo kwa miundombinu imara ya uchukuzi na usafirishaji wa watu na bidhaa. Pia, inakejeli kuwapo kwa miundombinu hafifu ya usafirishaji na uchukuzi wa anga, majini na nchi kavu. Dhamira hiyo inasisitiza kuwapo kwa miundombinu imara ili kuchochea kasi ya maendeleo.

Vilevile, suala la Kabuli kuchukuliwa na mkondo wa mto kwa muda wa saa kumi tu badala ya miaka kumi kama angetembea kwa miguu linaibua dhamira inayoonesha kuwapo kwa miundombinu hafifu katika jamii. Kwa kawaida, si rahisi safari yenye umbali wa miaka kumi kwa mguu ikachukua saa kumi tu. Kasi ya mkondo wa maji inayoelezwa inaweza kulinganishwa na kuwapo kwa reli za kisasa zinazotumia umeme, usafiri wa ndege na barabara imara zinazoweza kurahisisha wananchi kutimiza majukumu yao kwa wakati. Suala la ujenzi wa barabara imara, reli za kisasa na kuimarishwa kwa usafiri wa maji na anga linapaswa kupewa kipaumbele ili kurahisisha miundombinu hiyo kutimiza majukumu yake kwa wakati sahihi (Murry, 2023). Pia, kuimarika kwake

kunapaswa kwenda sambamba na upanuzi wa viwanja vya ndege, bandari, madaraja na barabara zitakazohimili mahitaji ya wananchi.

Fantasia nyingine iliyotumika kuibua dhamira ya ukosefu wa vyombo vya usafiri wa anga katika kitabu teule ni ile inayoonesha chombo alichotumia Amini kuzuru Ardhi. Amini, mjumbe aliyetumwa kuzuru Ardhi, hakuwa na namna salama ya kusafiri kwa kuwa nchi yake ilikuwa inaelea hewani kama wingu. Amini alishuka katika Ardhi kwa msaada uliopatikana kupitia ndege aliyejulikana kwa jina la Mangera. Uhusiano wa kimataifa ulififia katika nyanja zote za kijamii kama vile biashara na uchumi, diplomasia, michezo, tiba, elimu, sayansi na teknolojia. Raia wake walishindwa kuingiza na kutoa bidhaa zao. Mwandishi anaeleza kuwa usafiri wa anga katika nchi ya Kusadikika ulikuwa umefunga mahusiano na mawasiliano na mataifa jirani. Anaeleza:

> Amini alishuka katika Ardhi kwa msaada uliopatikana kwa hila kwa Mangera, ndege mkubwa kabisa walishao katika Ardhi, lakini walalao Kusadikika. Wakati wa kwenda chini Amini alijifunga bila ya kujulikana juu ya paja la Mangera aliyekuwa amelala fofofo usiku. Kulipokucha, ndege huyo aliamka akaruka mpaka chini. Alitua ziwani. Nusu ya mapaja yake ilikuwa majini. Kwa hivi amini alijifungua, akaogelea bila ya kuonekana mpaka ufukoni (uk. 40).

Nukuu hii inaonesha matumizi ya hali ya juu ya fantasia yanavyoibua dhamira ya ukosefu vyombo vya usafiri wa anga katika nchi ya Kusadikika. Amini alishuka katika Ardhi kwa msaada uliopatikana kwa hila kwa Mangera, ndege mkubwa kabisa wanaokula katika Ardhi, lakini wanalala Kusadikika, nchi inayoelea katika hewa kama wingu. Wakati wa kurudi, Amini alijifunga tena juu ya paja la Mangera aliyekuwa anashughulika na kula karamu ya mzoga wa ndovu bila ya kutazama huku wala huko. Jambo hili si rahisi kufanyika. Safari hizi ni za kifantasia zinazothibitisha kukosekana kwa vyombo vya usafiri wa anga. Ufafanuzi wa fantasia hiyo umemakinikia misingi ya nadharia teule inayozingatia ufumbuzi wa ishara wa mambo yanayojitokeza katika fasihi kwa kurejelea umathilishaji wa mazoea ya mazingira na maisha ya jamii. Taifa likikosa miundombinu imara ni jambo linalotia shaka katika harakati za maendeleo na uhusiano wake na mataifa mengine ya ulimwengu (Shivji, 2009; Utouh, 2022). Suala hili halipaswi kufumbiwa macho katika harakati za maendeleo ya binadamu za kuyamudu maisha na mazingira yake.

Njia za uchukuzi na usafirishaji wa anga, nchi kavu na maji ni moyo wa uchumi na maendeleo ya kila taifa. Kuimarika kwa miundombinu husika kunatokana na kukomaa kwa utashi wa viongozi katika usimamizi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo (Makoye, 1996). Ukosefu wa miundombinu unaweza kusababisha bidhaa ama mazao kuharibika na kutofika kwa wakati katika masoko husika. Uhaba na udhaifu wa miundombinu ya usafirishaji huchelewesha mwendo wa kufanya uchukuzi wa bidhaa (Makoye, 1996). Hakuna bidhaa au kitu kinachoweza kuingia wala kutoka nchini kwa wakati mwafaka kama njia za

usafirishaji na uchukuzi si imara. Nchi kama ina mazao mengi lakini haina njia za kuyapeleka katika masoko makubwa, faida haiwezi kupatikana kwa urahisi.

### 3.3 Fantasia Inayoonesha Uadui na Chuki

Suala la uhusiano mwema, umoja na ushirikiano katika jitihada za binadamu za kuyamudu maisha na mazingira yake ni la msingi. Hakuna maendeleo yanayoweza kufikiwa katika taifa lolote bila kuchukua hatua za kujenga umoja na ushirikiano katika jamii. Suala hilo linatazamwa kama nguzo ya kufanikisha maendeleo katika nyanja zote za kijamii. Umoja huleta tija na ufanisi katika shughuli zote za kijamii (Liundi, 2015). Kwa kurejelea riwaya teule, fantasia iliyotumika kuibua dhamira ya umoja na mshikamano ni ile inayoonesha namna serikali ilivyofanya jitihada za kuliondoa neno uadui katika lugha na vitabu vyao. Mwandishi anaeleza kuwa kwa amri ya serikali, matangazo yalienezwa katika njiapanda, barabara kuu na kila mahali pa mikutano ya watu ili kuzuia matumizi ya maneno neno uadui na mengine mabaya kama yanavyojulikana (uk. 18). Jitihada za kuzuia matumizi ya maneno mabaya zinaibua dhamira ya umoja na mshikamano katika jamii.

Matumizi ya fantasia pia yanaibua dhamira ya uadui na chuki inayoonesha nia ya serikali ya kutokomeza maovu nchini. Kwa mfano, mwandishi anaeleza kuwa serikali haina budi kuepuka uchokozi na kuviapiza vita kama laana inayopita kiasi kwa binadamu aliyejaliwa busara na haki, moyo wa wema, ulimi wa nasaha, masikio ya kusikilizana, macho ya uongozi, pua ya kutambua uovu na ushirika wa amani (uk. 17). Pia, anasisitiza kuwa siasa kubwa na bora ilenge kuwaunganisha watu wote katika misingi ya umoja na ushirikiano. Suala la uchokozi wa vita linapaswa kukemewa kwa nguvu kubwa kwa kuhimiza amani katika maisha ya binadamu (Mpangala, 2007). Uhusiano mwema unaelezwa kama wenzo wa kuwaunganisha binadamu katika taifa lao.

Pia, mwandishi ametumia kipengele cha fantasia kuibua dhamira ya mafunzo yaliyoambatanishwa na siasa ya urafiki katika nchi za Mashariki ya Kusadikika. Suala la kuimarika kwa mafunzo yaliyoambatana na siasa ya urafiki katika nchi za Mashariki linaelezwa kwa utaratibu mwingine: kama mtalaamu akikaa na mjinga, wa kwanza lazima amshirikishe wa pili katika elimu; na kama tajiri akikaa na maskini, wa kwanza afanye awezavyo kwa kumsaidia wa pili kwa utajiri wake; ulikuwa katika orodha ya mafunzo katika vyuo vingine (uk. 18). Maelezo hayo yamejengwa kifantasia kuibua dhamira ya urafiki ulivyokuwa umeimarishwa katika nchi za Mashariki. Kwa mfano, mwandishi anaeleza jinsi wataalamu na matajiri walivyotumia nafasi zao kuwainua kiuchumi na kielimu wenzao. Ushirikiano huo unasititiza kuwapo kwa matumizi sawia ya rasilimali za umma kwa masilahi mapana ya maendeleo ya taifa.

### 3.4 Fantasia Inayoonesha Wanawake wote Kuzaa Watoto Pacha

Dhamira ya inayohusu masuala ya uzazi na malezi imeibuliwa pia kupitia matumizi ya fantasia katika kitabu teule. Mojawapo ya misingi ya kuwapo kwa

uendelevu wa uzazi katika jamii ni ndoa. Ndoa ni ukamilifu wa makubaliano ya muungano kati ya mwanamume na mwanamke kuishi pamoja kulingana na sheria, mila na desturi za jamii inayohusika. Kila jamii ina utaratibu wake unaohusiana na masuala ya urafiki, uchumba na ndoa (Ismail, 2015). Mkataba huo unahitaji uaminifu, uadilifu na heshima kwa pande zote mbili ili udugu ushikamane na kuleta furaha. Kupitia mkataba huo, Mwenyezi Mungu anaweza kuwajalia zaidi kwa kuwapatia watoto wanaongeza furaha katika maisha ya ndoa (Muthubi, 2005). Fantasia iliyotumika kuibua dhamira ya uzazi na malezi ni ile inayoeleza kuwa wanawake wote katika nchi hiyo huzaa watoto pacha. Dhamira ya uzazi imewasilishwa kwa matumizi ya fantasia ya hali ya juu kama mwandishi anavyodokeza kuwa hii ni habari ya ajabu sana, lakini haionekani kuwa imepata kugusa ndoto za wazee. Mwandishi anaeleza :

> Wanawake wote katika nchi hiyo huzaa watoto pacha. Hii ni habari ya ajabu sana, lakini haionekani kuwa imepata kugusa ndoto za wazee. Wasimulizi bado kuisimulia, wala haijawashawishi wapima kuitia nchi hiyo katika ramani (uk. i).

Nukuu hii inaonesha matumizi ya fantasia yanavyoibua dhamira ya uzazi na malezi katika nchi ya Kusadikika. Upo ugumu wa kuamini kama kweli wanawake wote huzaa watoto pacha katika taifa hilo. Hata hivyo, dhamira hii inachunguza hali ya uzazi na ustawi wa watoto katika jamii za ulimwengu. Suala hilo linapaswa kuchunguzwa kwa mawanda mapana kwa manufaa ya ustawi wa jamii na taifa endelevu. Mojawapo ya masuala yanayopaswa kupewa nafasi ya pekee ni kuimarishwa kwa miundombinu ya afya, hasa vifaa-tiba, maabara, mafunzo na semina za kutosha kwa wataalamu wa kada ya afya. Pia, wataalamu wa kada ya afya waendelezwe kielimu na kupewa semina za mara kwa mara ili kuwajengea uwezo wa kumudu mahitaji ya kasi ya maendeleo ya sayansi ya tiba dhidi ya maradhi yanayoibuka kila kukicha. Mambo yanayoelezwa hapa yanapaswa kujengwa katika misingi imara ya usimamizi wa serikali. Serikali inapaswa kutekeleza sera ya afya kwa vitendo ili kuimarisha nguvukazi nchini.

Pia, suala la uzazi na malezi bora kwa watoto linahimizwa kuanzia ngazi ya familia katika jamii nyingi hapa nchini. Wazazi hawana budi kushirikiana kwa hali na mali ili kuwalea, kuwakuza na kuwajenga watoto wao katika misingi imara ya kimaadili (Hobart, 2009). Licha ya kuwa kupata watoto ni suala la baraka, wapo wanaowatelekeza kutokana na kuwapo kwa sababu mbalimbali (Ngadala, 2003). Wengi wao huwatelekeza watoto wao mara tu baada ya kujifungua. Watoto wanaotelekezwa hulelewa katika mazingira magumu yenye uangalizi mdogo wa kiafya na kimalezi. Jambo hilo husababisha baadhi yao kutetereka kiafya na hata kupoteza maisha.

Suala la uzazi na malezi linahitaji umoja na ushirikiano katika ngazi ya familia. Ushirikiano katika malezi ni nyenzo muhimu katika harakati za kuwajenga watoto kimaadili. Ustawi na uendelevu wa jamii na taifa lolote duniani hutegemea

sana kuwapo kwa misingi imara ya uwekezaji kwenye malezi bora na endelevu ya watoto (Mwanza, 2011). Malezi bora yana mchango mkubwa katika kuimarisha misingi ya kimaadili. Kila mwanadamu hutengenezwa na maadili yaliyopo katika jamii yake iliyomkuza na kumlea. Kila hatua ya maisha ya binadamu ina athari zake katika jamii na taifa. Wajibu wa jamii ni kujenga misingi imara itakayoziba mianya inayosababisha kuporomoka kwa maadili na maendeleo katika jamii na taifa.

## 4.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza namna matumizi ya fantasia yanavyoibua dhamira katika riwaya teule ya *Kusadikika*. Matokeo yameonesha jinsi matumizi ya fantasia yanavyoibua dhamira zilizoshikamana vyema na utamaduni, maisha na mazingira ya jamii. Pia, hutazamwa kama kiungo thabiti cha kifani kinachojenga misingi ya kuifunza jamii na kuileta pamoja kifikra, kiitikadi na kiutamaduni. Fantasia zilizowasilishwa zimeibua dhamira zilizoonesha matendo ya msingi ya binadamu yanayojidhihirisha katika nyanja zote za maisha ya binadamu. Msuko wa fantasia umejengwa kwa mvuto wa kisanaa unaolenga kuihamasisha jamii kupata udhati wa dhamira zilizoibuliwa. Makala hii inapendekeza kuwa utafiti ufanyike zaidi katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili kuhusu matumizi ya fantasia yanavyofumbata masuala ya uchumi, siasa, utamaduni na falsafa na itikadi za jamii.

## Marejeleo


Herman, L. (2012). “Fantasia katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto.” *Kioo cha Lugha*. 10: 122-134.

Hobart, C. (2009). *A practical Guide to Child Observation and Assessment.* Cheltenham: Stanley Thrones publisher.

Ismail, Z. (2015). *Historia ya Fasihi ya WatotoTanzania: Maendeleo na Mafanikio*. Wasilisho katika Kongamano la CHAWAKAMA – Afrika Mashariki Lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Kyambogo Uganda.

Liundi, C. (2015). *Nukuu za Kiswahili za Mwalimu Julius K. Nyerere Kutoka Kwenye Hotuba na Maandiko*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers Limited.

Makoye, H. (1996). Tanzania Traditional Dances, Choreography and Communication in Urban. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mark, G. (1995). *Post Modern Semiotics: Material Culture and the Forms of Post Modern Life*. Oxford: Basil Blackwell.

Mpangala, G.P. (2007). “The Role of Civic Soiety in the 2005 General Election in Tanzania.” *Tanzania Journal of Development Studies.* 7 (2): 1-8.

Mukandala, R.S. na Gasavasi, C. (2000). *Governance and Development at the Grassroots in Tanzania*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Murray, A. (2000). *Public Sector Restructuring in Namibia – Commercialisation, Privatisation and Outsourcing: Implication for Organised Labour*. Windhoek: LaRRI.

Muthubi, F. (2005). *Mikakaki na Mbinu za Usimilishaji katika Fasihi ya Watoto*. Tasinifu ya umahiri. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mutua, J.M. na Furaha, C. (2014). "Fani za Fasihi Zinazoibua Fantasia katika Hadithi za Watoto za Nyambura Mpesha." *Nordic Journal of African Studies*. 23 (4): 292-306.

Mwanza, P. (2007). *Mtindo wa Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea*. Tasinifu ya umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nazarova, T. (1996). *Linguistics and Literary Semiotics*. Moscow: Moscow State University Press.

Ngadala, D.K. (2003). "Mswada wa Ujenzi na Mmomonyoko wa Maadili ya Taifa: Mkutano wa Sekta ya Utamaduni" (Haujachapishwa). Morogoro.

Omary, M. (2011). Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Rajabu, A. (2012). Misemo ya Kiswahili katika Vazi la Fulana: Uchambuzi wa Dhamira na Matumizi ya Lugha. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ramadhan, H.A. (2018). *Diwani ya Una Nini*? Songea: Peramiho Printing Press.

Robert, S. (1991). *Kusadikika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Shivji, I. (2009). *Accumulation in An African Periphery*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Tehenan, M. (2003). *Maisha na Mafanikio*. Dar es Salaam: Jitambue Media Co. Limited.

Utouh, F. (2022). *Wari wa Uhuru*. Dar es Salaam: Delecom Publisher.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*, *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wanjala, S.F. (2013). *Kitovu cha Fasihi Simulizi: Kwa Shule, Vyuo na Ndaki.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.